# eGA INAVYOTIMIZA MAONO YA MWALIMU NYERERE

**Na WILLIAM SHECHAMBO**

TEKNOLOJIA ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ina nafasi kubwa ya kufanikisha mabadiliko ya kiuchumi kwa kuboresha maisha na kuleta maendeleo kwa wananchi wa maeneo yote mijini na vijijini.

Maendeleo hayo yatokanayo na TEHAMA ni sehemu ya utekelezaji wa maono ya muasisi wa taifa letu Hayati Mwalimu Julius Nyerere ambaye alipigania maendeleo yenye usawa kwa wananchi wote wa mijini na vijijini.

Itakumbukwa enzi za uhai wake, Mwalimu Nyerere ambaye mwaka huu taifa linakumbuka miaka 23 ya kifo chake, kilichotokea Oktoba 14, mwaka 1999, aliamini katika maendeleo ya watu na siyo vitu ili kila jamii iguswe popote ilipo.

Leo, maono haya yamefikiwa kutokana na uwepo wa teknolojia bunifu, ambazo huwezesha serikali kuhudumia wananchi wake kwa uwazi, urahisi, uharaka na ufanisi mkubwa, hii inasaidia kila mwananchi kupata huduma kwa usawa na kujiimarisha kiuchumi.

Mathalani, kupitia teknolojia wakulima hupata taarifa ya masoko ya bidhaa zao na huduma mbalimbali za kijamii zinazowezesha kuwainua wananchi kiuchumi katika shughuli zao za kila siku za kujiongezea kipato tena kwa usalama na uhakika.

Ili kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya teknolojia inayokua kila siku kote duniani, Serikali imeipa jukumu Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) la kukuza na kusimamia jitihada za serikali mtandao ikiwa ni pamoja na kubuni mifumo tumizi ya TEHAMA inayolenga kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

Mamlaka ya Serikali Mtandao ni taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019, inayoipa mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao na kuhimiza utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao kwa taasisi za umma.

Kimsingi kuanzishwa kwa e-GA mwaka 2019, kunaendeleza afua za iliyokuwa Wakala ya Serikali Mtandao na kuchukua sehemu ya mipango yake kwa sababu majukumu ya taasisi hizi yanafanana ingawa yanatofautiana katika mamlaka ya utendaji.

"Mamlaka ya Serikali Mtandao ni taasisi iliyoirithi Wakala ya Serikali Mtandao iliyoundwa Aprili 2012 kwa Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 Sura ya 245 ya mwaka 1997 yenye jukumu na mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za serikali mtandao nchini Tanzania," anasema Raphael Rutaihwa, Meneja wa huduma za Sheria e-GA.

Rutaihwa anaeleza kuwa, kabla ya kuanzishwa Wakala ya Serikali Mtandao, matumizi ya TEHAMA serikalini yalikuwa yanaratibiwa na kusimamiwa na Idara ya Usimamizi wa Mifumo (DMIS) iliyopo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambayo kwa sasa ni Idara ya Huduma za TEHAMA Serikalini (DICTS).

Hivyo, kwa mujibu wa Raphael, Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019 imeainisha majukumu na wajibu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao katika utekelezaji wa Serikali Mtandao nchini Tanzania.

Majukumu hayo yaliyogawanyika katika maeneo matatu, yanalenga kuziwezesha taasisi za umma kuboresha huduma zao ili kuwe na wepesi katika kuwahudumia wananchi mahali walipo kwa urahisi bila kuwalazimu kupoteza muda au kutumia rasilimali nyingine kufika ziliko ofisi za taasisi husika.

Katika kitabu chake "Binadamu na Maendeleo" kilichochapwa mwaka 1974, Mwalimu Julius Nyerere anasema "Watu wanapaswa kuhusishwa, ili kufikia maendeleo ya kweli". Katika nyakati hizi, njia mojawapo ya kuwahusisha watu ili kufikia maendeleo ya kweli kama anavyotuasa Baba wa Taifa ni kupitia TEHAMA.

Kupitia TEHAMA, wananchi wanaweza kuwasiliana na Serikali yao moja kwa moja; kupitia TEHAMA, wananchi wanaweza kutoa maoni na mawazo ya kujiletea maendeleo; kupitia TEHAMA wananchi wamewezeshwa kutoa taarifa mbali mbali za ukiukwaji wa sheria na taratibu mbali kama rushwa na makosa mengine ya jinai ambayo hudumaza maendeleo. Pia matumizi ya TEHAMA yamerahisisha na kuharakisha utoaji haki kwa wananchi.

"Tunaimarisha na kuendeleza utoaji wa huduma za Serikali Mtandao kwa taasisi za umma; Tunaimarisha uzingatiaji wa sera, sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao kwa taasisi za umma na pia tunaimarisha utafiti, ubunifu na uendelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao," anasema.

Raphael anasema, utekelezaji wa majukumu hayo makuu ya e-GA umefanikisha taasisi za serikali kuwahudumia wananchi mahali walipo kwa njia ya kidigitali, na hivyo kupunguza mzunguzo wa nyakara, hali iliyosaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti vitendo vya rushwa na urasimu.

"Nitolee mfano wa Mfumo wa Utoaji Huduma za Serikali kwa Simu, ambao unapatikana kwa namba ya msimbo ***152*00#,** unaowawezesha mwananchi mwenye simu ya mkononi, kupata huduma zinazotolewa na taasisi mbalimbali za serikali," anasema.

Kadhalika Raphael anasema, e-GA inatengeneza mifumo ya kidijitali yenye viwango kutokana na mahitaji ya serikali na jamii kwa wakati husika, ambapo wanajivunia timu ya wataalamu wabobezi waliopo katika mamlaka hiyo muhimu.

Pia anasema, pamoja na uwepo wa wataalamu hao, e-GA inaruhusu taasisi kujenga mifumo yao kulingana na mahitaji na aina ya huduma zao, lakini lazima izingatie viwango vilivyopangwa na mamlaka hiyo ili mifumo ionane na kubadilishana taarifa.

"Ili kufanikisha hili, tunazishauri taasisi za umma kuwa na vitengo vya TEHAMA vyenye wataalamu wenye sifa na pia kuwapa mafunzo kazini kadiri inavyoitajika kama sheria ya Serikali Mtandao inavyoagiza," anasema.

e-GA inafarijika kwakuwa serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, ipo tayari kuhakikisha jitihada za serikali mtandao zinafanikiwa kwa kuipa nguvu ya kisheria Mamlaka ya Serikali Mtandao pamoja na kuiwezesha kifedha ili kufikia malengo yake ya kujenga serikali ya Kidijitali, anasema Raphael.

"Rais Samia anasisitiza asilimia 40 ya maeneo ya umma kuwa na mawasiliano




mazuri katika kipindi cha miaka mitano ijayo na ameainisha maeneo ya kimkakati kuimarisha mawasiliano kuelekea katika uchumi wa kidijitali sambamba na kutoa fedha, hii ni faraja kwetu," anasema.

Raphael anaeleza kuwa, kutokana na utayari huo e-GA imedhamiria kufika maeneo mengi zaidi na hatimaye kuzifikia taasisi zote za umma, kutoka 300 hadi 350 zilizofikiwa sasa na huduma za mamlaka hiyo kati ya jumla ya taasisi 800 zilizopo.

"Hadi sasa tuna mifumo ya kifedha, mifumo ya kulipia ankara za maji na mfumo wa sekta ya afya upo njiani kukamilika, kiujumla tunaelekeza nguvu kubwa katika kubuni mifumo ya TEHAMA ya kisekta," anasema.

Meneja huyo anasema, ili kuongeza ufanisi wa taasisi hiyo katika kutekeleza majukumu yake, wameanzisha kituo maalumu cha utafiti na ubunifu ili kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi na serikali kwa ujumla.

"Kupitia kituo hiki, sasa tuko kwenye ukamilishaji wa mfumo wa kufuatilia utoaji wa ruzuku za kilimo za serikali, ili kuepusha urasimu ambao unaweza kujitokeza katika harakati za ugawaji wa mbolea kwa wananchi," anasema.

Raphael anatoa rai kwa taasisi zote za umma zenye mifumo yao, kuhakikisha zinawasilisha maandiko yao kwenye mfumo wa GISP ili iweze kupitiwa na kupatiwa ruhusa ya kuendelea nayo, kuifanyia maboresho na kama haikidhi viwango kuiacha kabisa.

Anasema, yote haya ni uthibitisho kuwa e-GA inatekeleza maono ya Mwalimu Nyerere enzi za uhai wake, ambaye aliamini katika maendeleo yenye usawa kwa wananchi wote vijini na mijini.

"Mwalimu alisema unaweza kuona Pato la Taifa limekuwa kumbe watu wanaomiliki uchumi ni wachache, yaani matajiri, huku wananchi wengi wako katika dimbwi la umasikini, sasa e-GA tunahakikisha kupitia teknolojia, wenye nacho na wasio nacho wote wanapata huduma sawa bila upendeleo," anasema.

"Kwa hiyo mwalimu alisema kipimo kizuri ni kwamba maendeleo lazima yahusishe watu, ni lazima kuyapima maendeleo hayo kwa kutathmini na kuona wananchi wengi wanaishi vipi; je, wanapata chakula bora? Wana makazi mazuri? Wana mavazi mazuri? Je, elimu yao ikoje? Na pia kuangalia upatikanaji wa huduma yao ya afya"

"Lakini ili uweze kupata maendeleo hayo, lazima uweke mazingira wezeshi, ikiwa ni pamoja na vitu vinavyochochea maendeleo. Vitu hivyo ni pamoja na huduma ya afya, elimu, maji na vyote vinavyogusa mwananchi moja kwa moja, dira ambayo ni msingi wa ufanyaji kazi wetu hapa e-GA," anasema.

Raphael anaongeza kuwa, Mwalimu Nyerere alikuwa anasisitiza kuwa kitu cha msingi katika kupima maendeleo ni lazima kiangalie maendeleo na jinsi huduma zinavyowafikia watu kama ambavyo e-GA inaendelea kufanya kila siku.

Leo hii, mwananchi kupitia mifumo rafiki iliyopo kwa uwezeshaji wa e-GA, anapata huduma zote mahali alipo bila usumbufu yakiwemo malipo ya ankara za maji na umeme, kodi za majengo, mapato na ardhi sambamba na kushikiri katika demokrasia.

